Zamani za kale mtu aliuliza**, “Kweli ni nini?”** (Yohana 18:38). Swali hili limerudiwa mara nyingi katika historia. Ulimwengu umejaa dini nyingi kwa haraka, na miongoni mwa dini hizi kuna maoni mengi. Ni ipi iliyo ya ukweli? Mwalimu mwenye busara alionya, **“Inunue ukweli, wala usiiuze”** (Mithali 23:23). Lakini, tutapataje ukweli huu katika mazunguko ya dini zilizopo? Ukweli unaweza kupatikana katika Biblia Takatifu, Neno la Mungu lililoandikwa.

## Neno la Mungu ni Kipimo cha Ukweli.

Yesu aliomba, **“Uwatakase kwa ile kweli; Neno lako ndiyo kweli”** (Yohana 17:17). **“Mungu wa Ukweli”** aliandika Biblia (Isaya 65:16; Zaburi 31:5). Hakika, Yesu alikiri kuwa **“njia, ukweli, na uzima”** (Yohana 14:6).

Ukweli wa Mungu huenezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine na unaletwa kwako leo. Kama Daudi, mtu aliyempendeza Mungu (1 Samueli 13:14), tunaamini kuwa **“Tazama wapendezwa na kweli iliyo moyoni”** (Zaburi 51:6). Kitabu hiki kimebuniwa kukusaidia kujipima ukitumia Neno la Mungu na **“...nitakuambia yaliyoandikwa katika maandiko ya kweli”** (Danieli 10:21).

Biblia inaeleza, **“Kwa kuwa hatuthubutu kujihesabu pamoja na baadhi yao wanaojisifu wenyewe, wala kujilinganisha nao, bali wao wenyewe wakijipima nafsi zao na nafsi zao, hawana akili”** (2 Wakorintho 10:12). Ni hatari kujipima kwa kile ambacho wengine wanaamini, au vile kanisa letu linavyosema.

Tunahitaji kujipima kwa Neno. Hatuwezi kuweka tumaini letu katika desturi kwani Biblia inaonya, **“Huku mkilitangua neno la Mungu kwa mapokeo yenu mliyopokeana; tena mwafanya mambo mengi yaliyo sawasawa na hayo”** (Marko 7:13). Imesemwa, “Kilicho cha kawaida siyo lazima kiwe kweli.”



Ed Cole alisema, “Kile mtu anachoamini huwa na nguvu ya wema au uharibifu katika maisha.” Kile tunachoamini kuhusu wokovu wetu ni cha maana sana kwani huamua mwisho wetu. Tunahiji kujirekebisha kulingana na ukweli wa Neno la Mungu. Kama mtu akisema jambo mbaya, kisha watu elfu moja wakisema kuwa ni sawa, bado ni mbaya.

Carlton L. Coon, Sr. katika mfululizo wake wa mafundisho ya Biblia unaoitwa, **Chukua Mizizi (Take Root)** anasema, “Kile watu wanachofundishwa, huamua wanachoamini. Wanachoamini, huamua wanachofanya. Wanachofanya huamua mwisho wao.”

Ni jinsi gani basi tunaweza kujipima wenyewe? Kweli, kwa Biblia! Kijitabu hiki kitakuongoza kupitia mafunzo ya msingi kukuonyesha jinsi unavyojipima kwa Neno la Mungu.

Kila fundisho linapozungumziwa, kuna hitaji la kuuliza swali, *“Je! Biblia inafundisha haya? Hivi ndivyo Maandiko yasemavyo?”* Hili ndilo swali la kwanza katika kuchunguza kila ujumbe, kipeperushi, au kitabu.

Biblia inasema wazi kuwa **“Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu”** (2 Timotheo 2:15). Kwa nini ujifunze? Ili **“kutumia kwa halali neno la KWELI.”** E. Stewart katika mafundisho yake, **“Ukweli Haubadiliki” (Truth Never Changes)** anatuambia kuwa Andiko hili linaeleza kuwa Neno linaweza **kutumiwa** vibaya.

**“Mkijua neno hili kwanza, ya kwamba hakuna unabii katika maandiko upatao kufasiriwa kama apendavyo mtu Fulani tu. Maana unabii haukuletwa popote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu”** (2 Petro 1:20-21).

Stewart alisema, “Katika 2 Petro 3:16 tunampata Petro akiandika kuhusu watu waliotumia maandiko vibaya au kupotosha na matokeo

ikawa uharibifu wao." Watu hawa ni wale "**wasio na elimu na wasio imara"** ambao huyapotoa (maana kuondoa maana ya, kugeuza au kutumia vibaya) **"...Maandiko kwa uvunjifu wao wenyewe."** Anaendelea kushauri, "Maisha yetu yafananishwe na Biblia badala ya Biblia kufanana na maisha yetu."

Hebu tuanze, **"Kuyachunguza maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayonishuhudia"** (Yohana 5:39).

**Sasa huu ni wakati wa kujitazama kwako kwa kwanza.**

Maswali matatu yatakusaidia kujipima kwa Neno la Mungu.

## Unajipimaje?

**Biblia ni kipimo cha ukweli.**

| | Ndiyo | Hapana | Sina Uhakika |
|---|---|---|---|
| Je! ni hivi ifundishavyo Biblia? | | | |
| Je! ni hivi kile unachoamini? | | | |
| Je! kanisa lako hufundisha hivi? | | | |

Neno la Mungu, lililovuviwa na Mungu, Neno la Mungu lina hakika. Mafundisho yawe na msingi juu yake, na kukubaliana na Neno la Mungu. Biblia haijavuviwa sehemu tu; yote imevuviwa. Maandiko **Yote** yamevuviwa na Mungu. Pia Biblia haina makosa. Hii inamanisha Roho Mtakatifu alipokuwa akitembea juu ya watu (2 Petro 1:20-21) uhaba na makosa ya waandishi haikupatikana. Waliweza kuandika bila makosa. Biblia inaweza kuaminiwa katika mambo yote ya imani.

√ "Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza,na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema" (2 Timotheo 3:16-17).



Neno **"vuviwa"** katika Maandiko linatokana na neno la Kigiriki linalomaanisha, **"pumzi ya Mungu."**

√ "Maana neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo" (Waebrania 4:12).

√ "Mbingu na nchi zitapita; lakini maneno yangu hayatapita kamwe" (Marko 13:31).

√ "Matendo ya mikono yake ni kweli na hukumu, maagizo yake yote ni amini, Yamethibitika milele na milele, yamefanywa katika kweli na adili. Amewapelekea watu wake ukombozi, Ameamuru agano lake liwe la milele, jina lake ni takatifu la kuogopwa" (Zaburi 111:7-9).

√ "Majani yakauka, ua lanyauka; bali neno la Mungu wetu litasimama milele" (Isaya 40:8).

√ "Bwana asema hivi, Simameni katika njia kuu, mkaone, mkaulize habari za mapito ya zamani, I wapi njia iliyo njema? Mkaenende katika njia hiyo, nanyi mtajipatia raha katika nafsi zenu. Lakini walisema, Hatutaki kwenda katika njia hiyo" (Yeremia 6:16).

√ "Kitabu hiki cha torati kisiondoke kinywani mwako, bali yatafakari maneno yake mchana na usiku, upate kuangalia kutenda sawasawa na maneno yote yaliyoandikwa humo; maana ndipo utakapoifanikisha njia yako, kisha ndipo utakapositawi sana" (Yoshua 1:8).

Jerry Vines na Jim Shaddix katika kitabu chao **"Nguvu za Madhababu" (Power in the Pulpit)** anatoa manufaa mengi ya Neno la Mungu. Orodha hii ina:

1. Ufanisi na kufaulu kwa wale wanaolitii Neno (Yoshua 1:8).
2. Hubadilisha nafsi, humtia mjinga hekima, huupa moyo furaha, huyatia macho nuru (Zaburi 19:7-8).
3. Neno ni la milele, kweli, haki, lina thawabu nyingi, na tamu. Hutoa onyo na thawabu (Zaburi 19:11).
4. Neno hututakasa na kutusaidia kuepuka dhambi (Zaburi 119:9-11).
5. Hutoa mwongozo na mwelekeo (Zaburi 119:105).
6. Neno ni Kweli (Yohana 17:17).
7. Matokeo huleta imani (Warumi10:17).
8. Maandiko hutoa hekima, mafundisho kuhusu kilicho sahihi, hukemea katika mabaya, hurekebisha waliokosa, na kuwaadibisha wale waliokosea, na kongoza. Haya yote hutusaidia kukomaa (2 Timotheo 3:14-17).
9. Neno li hai, kali, hupenya, na hutambua mawazo yetu na makusudi (Waebrania 4:12).
10. Hutupa lishe ya kiroho (2 Petro 2:2).

## Unajipimaje?

**Biblia imevuviwa, haina kosa, ina kweli na muhimu kwa watu wote.**

| | Ndiyo | Hapana | Sina Uhakika |
|---|---|---|---|
| Je! ni hivi ifundishavyo Biblia? | | | |
| Je! ni hivi kile unachoamini? | | | |
| Je! kanisa lako hufundisha hivi? | | | |



Kutoka mwanzo Mungu alikuwa na mpango. Alikuwa na lengo katika mawazo yake kwa ajili ya viumbe Vyake. Mungu hakuumba mashine. Viumbe Vyake vilikuwa na uwezo wa kuchagua na kufanya maamuzi kauli. Alipoumbwa mwanamume na mwanamke wa kwanza, Adamu na Hawa, aliwapa sharti moja. Wasile kutoka katika mti wa maarifa wa mema na mabaya uliokuwa katika shamba la Edeni. Mungu alizungumza na neno Lake lilikuwa wazi. Walikuwa na mashaka na neno la Mungu na kutenda jambo ambalo Aliwaagiza wasitende. Dhambi (1 Yohana 3:4; 5:17) ilileta mtengano na kuvunja uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu (Zaburi 66:18; Isaya 59:2). Mungu asingekwenda kinyume na neno lake na ilimbidi aweke ahadi Yake ya kifo. Ni gharama kubwa sana kulipa kwa ajili ya tunda tu. Kwa sababu ya kutotii kwao dhambi iliingia ulimwenguni. Kutoka wakati huo kila mtu alitungwa mimba katika dhambi.

- √ “Kwa hiyo, kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti; na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi” (Warumi 5:12).
- √ “Kama ilivyoandikwa hakuna mwenye haki, hata mmoja” (Warumi 3:10).
- √ “Kwa sababu wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu” (Warumi 3:23).
- √ “Kila lisilo la haki ni dhambi, na dhambi iko isiyo ya mauti” (1 Yohana 5:17).
- √ “Tazama, mimi naliumbwa katika hali ya uovu; mama yangu alinichukua mimba hatiani” (Zaburi 51:5).
- √ “Maana kila kilichomo duniani, yaani, tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, havitokani na Baba, bali vyatokana na dunia” (1 Yohana 2:16).

- √ "Lakini andiko limeyafunga yote chini ya nguvu ya dhambi, makusudi hao waaminio wapewe ile ahadi kwa imani ya Yesu Kristo" (Wagalatia 3:22).

- √ "Basi yeye ajuaye kutenda mema, wala hayatendi, kwake huyo ni dhambi" (Yakobo 4:17).

- √ "Kwa sababu kama kwa kuasi kwake mtu mmoja watu wengi waliingizwa katika hali ya wenye dhambi, kadhalika kwa kutii kwake mmoja watu wengi wameingizwa katika hali ya wenye haki" (Warumi 5:19).

**Mungu Anachukia dhambi. Walakini, Anampenda mwenye dhambi.**

- √ "Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi" (Warumi 5:8).

Kwa upande mwingine, Mungu ni wa rehema, na hataki kumwadhibu mwanadamu. Kwa upande mwingine, Mungu ni wa haki, na lazima aidhibu dhambi.

- √ "Mwenye kuwaonea huruma watu elfu elfu, mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi; wala si mwenye kumhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia kamwe" (Kutoka 34:7).

## Unajipimaje?

**Mwanadamu amezaliwa akiwa mwenye dhambi.**

| | Ndiyo | Hapana | Sina Uhakika |
|---|---|---|---|
| Je! ni hivi ifundishavyo Biblia? | | | |
| Je! ni hivi kile unachoamini? | | | |
| Je! kanisa lako hufundisha hivi? | | | |



Mwanadamu anahitaji mkombozi. Bila mkombozi anabaki kuwa mwovu, bila tumaini la maisha ya milele. Mwanadamu hawezi kujiokoa. Kiwango cha Mungu kinahitaji ukamilifu. Yesu alisema,**"Basi ninyi mtakuwa wakamilifu kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu"** (Mathayo 5:48). Wokovu hauwezi kununuliwa (Waefeso 2:8-9).

Ralph Vincent Reynolds alieleza hali ya mwanadamu ya huzuni.

- √ Amepotea tangu tumboni (Zaburi 58:3).
- √ Aliumbwa katika hali ya uovu (Zaburi 51:5).
- √ Moyo huwa mdanganyifu kuliko vitu vyote (Yeremia 17:9).
- √ Kuongozwa na Shetani (Waefeso 2:2).
- √ Sheria ya dhambi na kifo huendelea kufanya kazi katika maisha yake (Warumi 7:23).
- √ Chini ya laana (Wagalatia 3:10).
- √ Akili zimetiwa giza (Waefeso 4:18).
- √ Ana mawazo machafu (Mwanzo 6:5).
- √ Amejawa na udhalimu (Warumi 1:29).
- √ Wafu katika makosa na dhambi (Waefeso 2:1).
- √ Ameharibika tangu wayo wa mguu (Isaya 1:6).

## Unajipimaje?

**Mwanadamu Anahitaji mwokozi wa Kumkomboa kutoka hali yake isio na tumaini**

| | Ndiyo | Hapana | Sina Uhakika |
|---|---|---|---|
| Je! ni hivi ifundishavyo Biblia? | | | |
| Je! ni hivi kile unachoamini? | | | |
| Je! kanisa lako hufundisha hivi? | | | |

Mungu aliandaa suluhisho la tatizo la mwanadamu. Aliuvaa mwili, na kuja duniani kama Mwokozi. Alikufa Kalvari msalabani na kufufuka tena. Hii ililipa deni na adhabu ya dhambi za mwanadamu.

**“Kwa maana Mungu aliupenda ulimwengu sana akamtoa Mwana wake wa pekee, ili yeyote amwaminiye asiangamie, bali awe na uzima wa milele”** (Yohana 3:16). Katika Yohana 3:15-18, neno pamoja na chimbuko la neno **“amini”** limetumiwa mara tano tofauti. Lazima mwanadamu aamini kuwa Yesu Kristo ni Mwokozi ili kuokolewa. Malaika alimwambia Mariamu, **“Nawe utamwita YESU: maana atawaokoa watu wake kutoka dhambi zao”** (Mathayo 1:21). Yohana Mbatizaji alimwona Yesu akija na kukiri, **“Tazama Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhamb ya ulimwengu!” (Yohana 1:29).** Yesu alikuja ili, “**wote wapate kuamini kwa yeye”** (Yohana 1:7).

- √ “Yesu akamwambia, mimi ndimi huo ufufuo, na uzima. Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi” (Yohana 11:25).

- √ “Kwa sababu msiposadiki ya kuwa mimi ndiye, mtakufa katika dhambi zenu” (Yohana 8:24).

- √ “Kwa jina lake kila amwaminiye atapata ondoleo la dhambi” (Matendo 10:43).

Ni muhimu tuamini Yesu Kristo ni Mwokozi wetu. Kumkana Yesu Kristo ni kukana **“Ukweli”** wenyewe (Yohana 14:6).

## Unajipimaje?

**Lazima Mwanadamu amkubali Yesu Kristo kuwa Mwokozi ili kuweza kuokoka.**

| | Ndiyo | Hapana | Sina Uhakika |
|---|---|---|---|
| Je! ni hivi ifundishavyo Biblia? | | | |
| Je! ni hivi kile unachoamini? | | | |
| Je! kanisa lako hufundisha hivi? | | | |



“Rudia nyuma yangu ‘Nampokea Yesu Kristo kuwa Mwokozi wangu.’ Sasa, umeokoka.” Je! umesikia haya mara ngapi? Je! wewe umeyasema mara ngapi? Wazo hili linaonyesha, “amini tu na utaokolewa.” Kuna matatizo kadhaa katika aina ya mawazo kama haya.

Kwanza, kama vile A. W. Tozer alivyosema, inahitajika “Yesu asimame akingojea uamuzi wetu badala ya mioyo iliyohuzunika kungojea uamuzi wake kwetu.” Picha hapa inaonyesha Yesu akisimama mbele yetu, tulio hakimu. Akisha tazama ushahidi wote, na kungojea (na kutumaini) kuwa utatoa uamuzi, “Ninaamini. Ninakubali.” Mwanadamu yuko hivyo; anataka kila mara awe mwenye mamlaka. Tumepewa uhuru wa kufanya uamuzi wetu, lakini Mungu yuko mamlakani. Yesu alisema, **“Si ninyi mlionichagua mimi, bali ni mimi niliyewachagua ninyi”** (Yohana 15:16). Baadaye akasema, **“Niliwachagua katika ulimwengu”** (Yohana 15:19). Ni Mungu atakaye tuhukumu. Paulo alisema Bwana ni **“Mhukumu Mwenye Haki”** (2 Timotheo 4:8). **“Bwana atawahukumu watu wake. Ni jambo la kutisha kuanguka katika mikono ya Mungu aliye hai”** (Waebrania 10:30-31).

Ni jambo la kawaida leo kusikia wahubiri wakihimiza watu ‘kumpokea’ Bwana awe kama Mwokozi wao. Raymond Woodward katika nakala yake, **Toba Ni Nini (What is Repentance)** anasema, “Biblia haizungumzii kuhusu sisi ‘kumpokea” Bwana. (Hakika, tunastahili kushukuru milele kuwa Alichagua kutukubali!)”

Biblia inafundisha kuwa kubadilishwa kamili hakuwezi kutendeka bila toba. Yesu alifundisha, **“Nawaambia, sivyo; lakini msipotubu, ninyi nyote mtaangamia vivyo hivyo”** (Luka 13:3).

Yohana Mbatizaji alikuja akihubiri toba (Mathayo 3:1-2). Pia Yesu Kristo alianza huduma yake kwa mwito wa “toba.”

**“Tokea wakati huo Yesu alianza kuhubiri, na kusema, tubuni, kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia”** (Mathayo 4:17).

Kabla ya kwenda mbinguni Yesu aliwakumbusha wanafunzi wake **“Na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanzia tangu Yerusalemu”** (Luka 24:47).
**“Basi zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni; bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu”** (Matendo 17:30). Hii inajumuisha wote. Alisema, “**watu wote kila mahali”**

**“Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu yeyote apotee, bali wote wafikie toba”** (2 Petro 3:9).

Mungu aliona ni muhimu toba ihubiriwe katika kila taifa. Hitaji la toba ni kwa wote kwa sababu dhambi iko katika watu wote. Dhambi imegusa maisha ya kila mwanadamu.

Toba hutendeka tunapo “ungama” dhambi zetu. “Kuungama kwa kweli ni wakati tunaposema jambo sawa na vile Mungu anavyosema kuhusu dhambi zetu.” **(Urahisi wa Wokovu, The Simplicity of Salvation)**

**“Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote”** (1 Yohana 1:9).

Woodward anafafanua toba ya ki-Biblia kuwa “mbadiliko wa NIA ya ndani ambayo huongoza badiliko la TENDO. Yote mawili yasipotendeka, toba ya kweli haijapatikana.”

Toba ni hatua muhimu katika mpango wa wokovu. Ni hatua ya kwanza ya mwanadamu kumwelekea Mungu na msamaha wa dhambi. Petro alisema, **“Tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu”** (Matendo 2:38).



Eddie Jones katika **Ukweli kuhusu Toba (The Truth About Repentance)** anaandika “Hali ya toba siyo tu kugeuka kutoka, lakini pia kuelekea. Kutasababisha mtu kuacha tendo baya na kuanza kutenda mema.”

Toba inahushisha kugeuka kutoka ka dhambi, kumgeukia Mungu. ni hatua ya kugeuka katika maisha. Mtu anatembea katika njia moja, njia ya dhambi, ana “geuka kabisa” na kuanza kwende njia nyingine kumwelekea Mungu. Toba ni “kugeuka kutoka kwa njia uliyokua ukiendea; kumwomba Mungu akusamehe.”

- √ “Lakini mtu mbaya akighairi, na kuacha dhambi zake zote alizozitenda, na kuzishika amri zangu zote, na kutenda yaliyo halali na haki, hakika ataishi, hatakufa (Ezekieli 18:21).

- √ “Aendaye kwa unyofu ataokolewa; bali mkaidi wa njia zake ataanguka mara” (Zaburi 28:18).

## Jinsi ya Kutubu?

Wema wa Mungu huongoza watu katika toba na wema huo usidharauliwe.

**“Au waudharau wingi wa wema wake na ustahimili wake na uvumilivu wake, usijue ya kuwa wema wa Mungu wakuvuta upate kutubu?”** (Warumi 2:4).

- √ Injili inahubiriwa (Warumi 10:14).
- √ Mwenye dhambi huchomwa moyo (Matendo 2:37).
- √ Anakubali ni mtenda dhambi (Warumi 3:23; 6:23).
- √ Anatambua kuwa Mungu amemtoa Mwokozi (Mathayo 1:21; Yohana 4:42).
- √ Anatubu (ungama) dhambi zake. Siyo tu kusikitika lakini anaamua kuziacha dhambi (Mithali 28:13; Isaya 55:7) na kumgeukia Mungu (Luka18:13).

## Mungu hufanya nini na dhambi zilizosamehewa?

- √ Huziweka katika vilindini vya bahari (Mika 7:19).
- √ Huzitupa dhambi zetu zote nyuma yake (Isaya 38:17).
- √ Hazikumbuki tena (Yeremia 31:34).
- √ Huziondoa mbali kama mashariki ilivyo mbali na magharibi (Zaburi 103:12).

## Unajipimaje?

**Biblia inafundisha kuwa kubadilika kwa kweli hakuwezi kuwepo pasipo toba.**

| | Ndiyo | Hapana | Sina Uhakika |
|---|---|---|---|
| Je! ni hivi ifundishavyo Biblia? | | | |
| Je! ni hivi kile unachoamini? | | | |
| Je! kanisa lako hufundisha hivi? | | | |

- √ "Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno, akamkirimia jina lile lipitalo kila jina" (Wafilipi 2:9).

- √ "Yesu akaja kwao, akasema nao, akwaambia, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani" (Mathayo 28:18).

- √ "Walipowaweka katikati wakawauliza, kwa nguvu gani na kwa jina la nani ninyi mmefanya haya?" (Matendo 4:7).

Jina Yesu lamaanisha **"Yehova Mwokozi"** au **"Yehova amefanyika wokovu wangu"** (Isaya 12:2). Je! jina la Yesu litumiwe lini? Swali bora zaidi linaweza kuwa, "Ni wapi ambapo hatutakiwi kutumia jina la Yesu?" mwandishi mmoja alisema, **"Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu baba kwa yeye"** (Wakolosai 3:17). Jina la **"Yesu"** limetajwa mara mia sita katika Biblia. Jina Lake linawakilisha nguvu kuu na mamlaka na linaweza kutumiwa:



- √ Katika maombi (Yohana 14:12-14).
- √ Katika kuhubiri (luka 24:47).
- √ Ukiwa na hitaji (Yohana 15:16).
- √ Katika uponyaji (Matendo 3:6, 16; Matendo 4:7, 10, 7-18).
- √ Unapokemea mapepo (Matendo 16:18).
- √ Kupokea uzima wa milele (Yohana 20:31).
- √ Katika wokovu (Matendo 4:12).
- √ Katika ubatizo wa maji (Matendo 2:38; 8:16; 10:48;19:5; 22:16)
- √ Katika kila jambo (Wakolosai 3:17).

## Unajipimaje?

**Kuna nguvu kuu na mamlaka katika jina la Yesu.**

| | Ndiyo | Hapana | Sina Uhakika |
|---|---|---|---|
| Je! ni hivi ifundishavyo Biblia? | | | |
| Je! ni hivi kile unachoamini? | | | |
| Je! kanisa lako hufundisha hivi? | | | |

Toba siyo kamili bila ubatizo. Biblia inafundisha kuwa tutubu na kubatizwa (Matendo 2:38; Luka 24:47; Marko 16:16). Toba na ubatizo huambatana pamoja. Zisitenganishwe. "Huendana pamoja, kufanikisha kazi kamili ya Mungu ya msamaha katika moyo wa mwamini." (Woodward, **Nini Hutendeka Katika Toba, What Happens at Repentance**).

## Kuamini huongoza kuelekea Ubatizo

- √ "Aaminiye na kubatizwa ataokoka" (Marko 16:16).

- √ "Lakini walipomwamini Filipo, akizihubiri habari njema za ufalme wa Mungu, na jina lake Yesu Kristo, wakabatizwa, wanaume na wanawake" (Matendo 8:12).

√ "Na ilikuwa Krispo, mkuu wa sinagogi, akamwamini Bwana pamoja na nyumba yake yote. Wakorintho wengi waliposikia, waliamini, wakabatizwa" (Matendo 18:8).

Katika kanisa la awali, watu walibatizwa mara tu wanapoamini. Filipo alimwambia Towashi wa Kushi anaweza kubatizwa ikiwa **"…unaamini kwa moyo wako wote, inawezekana"** (Mdo. 8:37).

Injili zinamalizia na agizo la Yesu kubatiza mataifa yote (Mathayo 28:19). Ujumbe wa kwanza kuhubiriwa na mitume, siku ya kuzaliwa kwa kanisa, matokeo yake ilikuwa agizo la kila mtu kubatizwa (Matendo 2:38). Kwa hivyo, ubatizo wa maji ni tendo la kutii amri ya Kristo.

Yesu alionyesha umuhimu wa ubatizo wa maji alipomwagiza Nikodemu, **"Amin, amini, nakuambia, mtu asipozaliwa kwa maji na kwa roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu"** (Yohana 3:5).

Matukio yote ya ubatizo katika Biblia ni kwa kuzamishwa (Yohana 3:23; Matendo 8:38; Warumi 6:4-5). Yesu Mwenyewe alitoa mfano kwa kuzamishwa (Mathayo 3:16). Neno ubatizo linatokana na neno la Kigiriki **"baptizo"** linalomaanisha kuchovya, kutumbukiza, kufunika. Kutumbukiza ni neno kubwa linalo maanisha kufunika kabisa kwa maji.

√ "Yohana naye alikuwa akibatiza huko Ainoni, karibu na Salimu, kwa sababu huko kulikuwa na maji tele; na watu wakamwendea, wakabatizwa" (Yohana 3:23).

√ "Akaamuru lile gari lisimame; wakatelemka wote wawili majini, Filipo na yule towashi; naye akambatiza. Kasha, walipopanda kutoka majini…" (Matendo 8:38-39).

√ "Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya



wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake" (Warumi 6:4-5).

## Ubatizo ni Muhimu Katika Wokovu

√ "Aaminiye na kubatizwa ataokoka" (Marko 16:16).

√ "Mfano wa mambo hayo ni ubatizo, unaowaokoa ninyi pia siku hizi; (siyo kuwekea mbali uchafu wa mwili, bali jibu la dhamiri safi mbele za Mungu), kwa kufufuka kwake Yesu Kristo" (1 Petro 3:21).

## Unajipimaje?

**Kuamini huongoza kuelekea ubatizo wa maji kwa kuzamishwa na ni muhimu katika wokovu**

| | Ndiyo | Hapana | Sina Uhakika |
|---|---|---|---|
| Je! ni hivi ifundishavyo Biblia? | | | |
| Je! ni hivi kile unachoamini? | | | |
| Je! kanisa lako hufundisha hivi? | | | |

Ron Schoolcraft katika **Kutazama Mathayo 28:19 Tena (A Fresh Look at Matthew 28:19)** anasema kuwa andiko hili ni bora zaidi katika Biblia kwa ubatizo katika jina la Yesu. Swali rahisi linaulizwa, "Jina ni lipi?" jibu ni rahisi, lakini la maana sana, "Yesu." Thibitisho kamili linapatikana katika Kitabu cha Matendo ambapo mitume walitii Mathayo 28:19 kwa kubatiza katika jina la Yesu!" **M**itume hawakuambiwa kunukuu utaratibu tu, vyeo au maneno. Waliambiwa kubatiza katika jina. Kila tukio la ubatizo katika Kanisa la Agano Jipya lilitekelezwa katika jina la Yesu. Petro, mhubiri wa

kwanza aliyepewa funguo za ufalme (Mathayo 16:18), alitumia jina la Yesu katika ubatizo.

√ "Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipwa cha Roho Mtakatifu" (Matendo 2:38).

√ "Kwa maana bado hajawashukia hata mmoja wao, ila wamebatizwa tu kwa jina lake Bwana Yesu" (Matendo 8:16).

√ "Akaamuru wabatizwe kwa jina lake Yesu Kristo. Ndipo wakamsihi azidi kukaa siku kadha wa kadha" (Matendo 10:48).

√ "Waliposikia haya wakabatizwa kwa jina la Bwana Yesu" (Matendo 19:5).

√ "Basi sasa, unakawilia nini? Simama, ubatizwe, ukaoshe dhambi zako, ukiliitia jina lake" (Matendo 22:16).

√ "Maana ninyi nyote mlibatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo" (Wagalatia 3:27).

√ "Na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu" (Luka 24:47).

## Kwa nini Yesu aliagiza kubatizwa "katika jina?"

√ Jina lake liko juu ya majina yote (Wafilipi 2:9-11; Waefeso 1:21).

√ Hakuna wokovu katika jina lingine (Matendo 4:10-12).

√ Lolote utendalo tenda kwa jina la Bwana Yesu (Wakolosai 3:17).

√ Tunaoshwa katika jina la Bwana Yesu (1 Wakorintho 6:11). **(Maswali Mawili Muhimu Katika Uhai, Kutafuta Ukweli, Two Important Questions in Life, Search for Truth)**



Paulo alikuwa na uhakika katika ubatizo katika jina la Yesu kuwa muhimu hali iliyompelea kuwabatiza tena waamini katika jina la Yesu (Matendo 19:1-5).

Ubatizo huondoa dhambi. Damu ya Yesu Kristo ni muhimu kuondoa dhambi. (Waebrania 9:22; 1 Yohana 1:7). Njia ya kipekee ya ki-Biblia kupokea ondoleo la dhambi ni kupitia ubatizo katika jina la Yesu (Luka 24:47; Matendo 2:38).

## Unajipimaje?

**Ubatizo wa maji unatakiwa utekelezwe katika jina la Bwana Yesu Kristo.**

| | Ndiyo | Hapana | Sina Uhakika |
|---|---|---|---|
| Je! ni hivi ifundishavyo Biblia? | | | |
| Je! ni hivi kile unachoamini? | | | |
| Je! kanisa lako hufundisha hivi? | | | |

Agano la Kale lina ahadi za kumwagwa kwa Roho Mtakatifu (Yeremia 31:33-34; Ezekieli 36:26-27; Yoeli 2:28-29). Roho wa Mungu angeishi ndani ya mwanadamu. Roho Mtakatifu alipomwagwa Siku ya Pentekoste, ilikuwa timizo la unabii wa Yoeli. Swali liliulizwa, **"Maana yake nini mambo haya"** (Matendo 2:12). Jibu, **"Lakini jambo hili ni lile lililonenwa kwa kinywa cha nabii Yoeli. Itakuwa siku za mwisho, asema Mungu nitawamwagia watu Roho yangu"** (Matendo 2:16-17).

Ishara ya ubatizo wa Roho Mtakatifu ni kunena kwa lugha nyingine, kama roho anavyowajalia.

## Faida ya kuwa na Roho Mtakatifu.

√ Hutufundisha mambo yote; hutupa ufahamu wa Neno (Yohana 14:26).
√ Huburudisha na kuwapa waliochoka pumziko (Isaya 28:12).
√ Hutoa nguvu ya kushuhudia (Matendo 1:8).
√ Hutoa ahadi kuwa tutafufuliwa (Warumi 8:11).

√ Hutusaidia katika maombezi (Warumi 8:26).
√ Kristo huweka mhuri wa kutumiliki (Warumi 8:9).
√ Atainua kiwango juu kinyume cha adui zetu (Isaya 59:19).

Mungu aliahidi na kutimiza ahadi Zake. (Warumi 4:21; Hesabu 23:19.) Ubatizo wa Roho Mtakatifu ni kwa **"yeyote"** (Matedno 2:21). Petro alikiri kuwa ahadi ya Roho Mtakatifu:

**"Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie"** (Matendo 2:39).

## Unajipimaje?

**Ubatizo wa Roho Mtakatifu ni ahadi kwako.**

| | Ndiyo | Hapana | Sina Uhakika |
|---|---|---|---|
| Je! ni hivi ifundishavyo Biblia? | | | |
| Je! ni hivi kile unachoamini? | | | |
| Je! kanisa lako hufundisha hivi? | | | |

√ "Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka" (Maatendo 2:4).

√ "Petro alipokuwa akisema maneno hayo Roho Mtakatifu akawashukia wote waliolisikia lile neno. Na wale waliotahiriwa, walioamini, wakashangaa, watu wote waliokuja pamoja na Petro, kwa sababu Mtaifa nao wamemwagiwa kipawa cha Roho Mtakatifu" (Matendo 10:44-45).

√ "Akawauliza, Je! Mlipokea Roho Mtakatifu mlipoamini? Wakamjibu, La, hata kusikia kwamba kuna Roho Mtakatifu hatukusikia. Akawauliza, Basi mlibatizwa kwa ubatizo gani? Wakasema, kwa ubatizo wa Yohana. Paulo akasema, Yohana alibatiza kwa ubatizo wa toba, akiwaambia watu wamwamini yeye atakayekuja nyuma yake, yaani, Yesu. Waliposikia haya wakabatizwa kwa jina la Bwana Yesu. Na Paulo, alipokwisha kuweka mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu akaja juu yao; wakaanza kunena kwa lugha, na kutabiri" (Matendo 19:2-6).



√ "Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya" (Marko 16:17).

√ "Na tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba yangu; lakini kaeni humu mjini, hata mvikwe uwezo utokao juu" (Luka 24:49).

## Unajipimaje?

**Kunena katika ndimi ni ishara ya kupokea Roho Mtakatifu.**

| | Ndiyo | Hapana | Sina Uhakika |
|---|---|---|---|
| Je! ni hivi ifundishavyo Biblia? | | | |
| Je! ni hivi kile unachoamini? | | | |
| Je! kanisa lako hufundisha hivi? | | | |

Wengine wanaweza kuuliza, "Je ni muhimu kubatizwa kwa Roho Mtaktifu?" Ikiwa ilikuwa muhimu kwa Mitume, Mariamu mama yake Yesu na wanafunzi wengine wa Yesu Kristo kuwa na Roho basi ni muhimu kwetu pia. Wanafunzi walitembea na Yesu, walishuhudia, walihubiri hata kukemea mapepo. Walitenda mambo haya makuu kwa sababu Yesu alikuwa nao. Walakini alipopaa, **"Msaidizi"** mwingine alitumwa (Yohana 14:16). **"Msaidizi"** huyu alikuwa ni sawa kuwa na Yesu akitembea pamoja nao tena. **"Kristo aliye ndani yenu, ni tumaini la utukufu"** (Wakolosai 1:27). Alikuja ndani yetu kupitia ubatizo wa Roho Mtakatifu.

Wazo la maana ni hili: **“Mtu asiye na Roho wa Kristo, huyo siyo wake”** (Warumi 8:9). Andiko hili linamaanisha kama hatuna Roho wa Kristo sisi siyo wa kwake.

**“Lakini ikiwa Roho yake yeye aliyemfufua Yesu katika wafu anakaa ndani yenu, yeye aliyemfufua Kristo Yesu katika wafu ataihuisha na miili yenu iliyo katika hali ya kufa, kwa Roho wake anayekaa ndani yenu”** (Warumi 8:11). Tutahitaji ubatizo wa Roho Mtakatifu ili kunyakuliwa.

Isaya alisema, **“hata Roho itakapomwagwa juu yetu kutoka juu”** (Isaya 32:15). Hii ndiyo sababu iliyomfanya Yesu awaagize wanafunzi wakae Yerusalemu hadi wapokee ahadi (Luka 24:49).

Yesu anataka kufungua milango ya mbinguni na kukupa Roho Mtakatifu. Anataka kukupa miminiko wa Roho. Baba yako wa mbinguni anajua jinsi ya kukupa thawabu nzuri. **“Kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao!”** (Luka 11:13).

**“Je! ulipoamini ulipokea Roho Mtakatifu?”** (Matendo 19:2). Tafsiri halisi ya swali hili ni, “Ulipoamini, ulipokea Roho Mtakatifu?”

## Unajipimaje?

**Ubatizo wa Roho Mtakatifu ni muhimu kwa mwamini.**

| | Ndiyo | Hapana | Sina Uhakika |
|---|---|---|---|
| Je! ni hivi ifundishavyo Biblia? | | | |
| Je! ni hivi kile unachoamini? | | | |
| Je! kanisa lako hufundisha hivi? | | | |

Moja wapo wa unabii muhimu katika Biblia ni kuwa Yesu anarudi hivi karibuni. Ni wokovu tu ambao umetajwa katika sehemu nyingi za Neno la Mungu.



Yesu Kristo alikwenda mbinguni kuandalia Wakristo nyumba ya milele. Mbinguni ni mahali palipoandaliwa kwa ajili ya watu waliojiandaa.

**“Nyumbani mwa Baba yangu mna makoa mengi; kama sivyo,ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi mwepo.” Yohana 14:2-3**

**“Wakasema, Enyi watu wa Galilaya, mbona mmesima mkitazama mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa \kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni.” Matendo 1:11**

Yesu atarudi upesi na kunyakua watu wake. Neno unyakuo humaanisha “kuondolewa” au “kutwaliwa juu.” Basi ni kuondolewa kwa kanisa, kutoka duniani, kukutana na Bwana hewani (1 Wathesalonike 4:13-18, 5:2-3; 1 Wakorintho 15:51-55).

## Unajipimaje?

**Yesu anarudi tena.**

| | Ndiyo | Hapana | Sina Uhakika |
|---|---|---|---|
| Je! ni hivi ifundishavyo Biblia? | | | |
| Je! ni hivi kile unachoamini? | | | |
| Je! kanisa lako hufundisha hivi? | | | |

**“Ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba; maana mlango ni mpana, na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa mlango huo. Bali mlango ni mwembamba, na njia imesonga iendayo uzimani, nao waionao ni wachache.”**
**Mathayo 7:13-14**

Andiko hili linahitimisha kuwa kuzimu kutakuwa na umati mkubwa kuliko mbinguni.

# Maamuzi ya leo yanaamua hatima ya kesho.

## Unajipimaje?

### Je! Uko tayari?

**Maswali machache ya mwisho.**

1. Je! uko katika hali ya kiroho mahali ambapo una uhakika kamili kuwa una uzima wa milele?
2. Je! kuna kitu kinacho kukandamiza au kukurudisha nyuma usiwe na uhakika kamili wa wokovu? Ikiwa kipo, ni nini?
3. Kwa hali isiyo tarajiwa ukifa katika usingizi wako usiku wa leo, utaamkia wapi?

**"Kwa kuwa Mungu hakutuweka kwa hasira yake, bali tupate wokovu, kwa Bwana wetu Yesu Kristo; ambaye alikufa kwa ajili yetu, ili tuishi pamoja naye, kwamba twakesha au kwamba twalala."**
**1 Wathesalonike 5:9-10**

Katika hali ya kujifunza kijitabu hiki maswali yanaweza kutokea. Tuko tayari kusaidia. Mwinjilisti alimwuliza Towashi wa Kushi, "Je! Yamekuelea haya unayosoma? Akasema, Nitawezaje kuelewa, mtu asiponiongoza? (Matendo 8:31). Andika maswali yako katika nafasi iliyotolewa. Mwalimu wa mafundisho ya Biblia atafurahi kukusaidia. Unaweza kutuandikia katika anwani iliyotolewa nyuma ya kitabu hiki.



# MASWALI

**Kwa Ajili ya Kujifunza Zaidi**

| | |
|---|---|
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |

Mwalimu wa Somo la Biblia ……………………..
Anwani ya Mawasiliano ………………………
Namba ya Simu ……………………………….

Apostolische Pfingstgemeinde Mannheim
Friedelsheimerstr. 18-20
D - 68199 Mannheim (Neckarau) /Germany
Pastor Raymond Wey
Assistent Pastor Sascha Wey
www.jesus-is-god.de, www.v-p-m.de